

UTAJUAJE KAMA WEWE NI MTUMISHI WA MUNGU NA KRISTO YU  
PAMOJA NAWWE?.

(Masomo maalumu kwa watumishi).

Jina la Mwokozi YESU KRISTO Lihimidiwe daima.

Je unajua namna yakujipima kama kweli wewe ni mtumishi wa Mungu na Kristo yu pamoja nawe?

Je unadhani ni ishara na miujiza ndio utambulisho pekee ya kwamba Kristo yu pamoja nawe?

Nataka nikuambie La!..Ishara na miujiza si uthibitisho wa kwanza wa Kristo kuwa pamoja nawe, kwasababu biblia inasema Yohana Mbatizaji hakufanya ishara hata moja lakini bado alikuwa mkuu kuliko manabii wote waliotangulia.

*Yohana 10:41 "Na watu wengi wakamwendea, wakasema, Yohana kweli hakufanya ishara yo yote, lakini yote aliyoyasema Yohana katika habari zake huyu yalikuwa kweli".*

Na pia wapo watakaofanya ishara lakini atawakana kuwa hawajui...

*Mathayo 7:22 “Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi?”*

*23 Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu”.*

Umeona kumbe kufanya ishara au kutofanya si tija!..Si uthibitisho wa kwanza kuwa Kristo yu nawe!.

Sasa ni kipi kinachotupa uthibitisho kuwa tunatembea na YESU katika utumishi tunaoufanya?.

Jibu tutalipata katika maandiko yafuatayo..

*Yohana 12:26 “Mtu akinitumikia, na anifuate; nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo. Tena mtu akinitumikia, Baba atamheshimu”.*

Hapo Bwana anasema mtu akitaka kumtumikia, yani kuwa mtumishi wake BASI AMFUATE!!... Na yeye alipo ndipo na mtumishi wake alipo, au kwa lugha nyepesi “Yeye yupo pamoja na wale waliomfuata”.

Sasa tunamfuata vipi YESU?.

Tusome tena maandiko yafuatayo..

*Luka 9:23 “Akawaambia wote, Mtu ye yote AKITAKA KUNIFUATA, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku, anifuate.*

*24 Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu ndiye atakayeisalimisha”.*

Kumbe ili tuwe watumishi wa kweli wa Mungu, ambao Kristo atakuwa nasi muda wote ni lazima TUJIKANE NAFSI KILA SIKU??.

Sasa swali ni je tumejikana nafsi zetu? au tunazipenda nafsi zetu na kuzishibisha kwa kila tunachokitaka.

UTAJUAJE KAMA WEWE NI MTUMISHI WA MUNGU NA KRISTO YU  
PAMOJA NAWWE?.

Huwezi kumtumikia Mungu na huku hutaki kuacha mila, huwezi kumtumikia Mungu na huku unaupenda ulimwengu.

Huwezi kuwa mtumishi wa Mungu na huku hutaki kuacha mizaha, na wala dhambi.

Huwezi kumtumikia Mungu na bado unaishi na mke/mume asiye wako. Fahamu kuwa Kristo hayupo na wewe hata kama unaona ishara na miujiza katika maisha yako..hiyo ni kulingana na maneno ya Kristo mwenyewe.

Kanuni ya kutembea na Kristo, itabaki kuwa ile ile MILELE! Nayo ni KUJIKANA NAFSI, KUBEBA MSALABA NA KUMFUATA YEYE!. Kwasababu Kristo ni yeye yule, jana na leo na hata milele (Waebrania 13:8).

Na hiyo ni kwa faida yetu na si yake! (*Ayubu 35:7*).

Huenda umeshamwamini Kristo kuwa ni Bwana na Mwokozi wa maisha yako!.. Hiyo ni nzuri sana, lakini bado haitoshi, ni lazima uongezee hapo "KUJIKANA NAFSI!". Na baada ya kufanya hivyo pia ujiandae kwa dhiki kwaajili yake.

Jiandae kuchekwa, kudharaulika, kuonekana mshamba, mjinga na usiyejielewa. Usiogope maana hizo ndizo chapa zake Yesu, (*Wagalatia*

UTAJUAJE KAMA WEWE NI MTUMISHI WA MUNGU NA KRISTO YU  
PAMOJA NAWWE?.

6:17), na wewe sio wa kwanza, zilianza kwa Kristo BWANA WETU NA  
AKAZISHINDA.

*Yohana 16:33 “Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani  
yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi  
nimeushinda ulimwengu”*

Bwana akubariki.

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255789001312 au +255693036618

Mafundisho mengine:

REKEBISHA YAFUATAYO ILI UCHUMI WAKO UKAE SAWA.

KAMA MTUMISHI WA MUNGU, TAFUTA MAARIFA KWA BIDII.

